Gazeti Makhsusi

GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXII Nam. 6485 **8 Julai, 2013** **Bei Shs. 5,000/=**
Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya kufuta na kuweka Sheria ya Biashara ya Zanzibar No. 4 ya 1989 na kuweka vifungu vya kuimarisha biashara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo..... 275

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada uliyotajwa hapo chini umetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya kufuta na kuweka Sheria ya Biashara Zanzibar.

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 12 Juni, 2013 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
8 Julai, 2013

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA

wa

MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA NA KUWEKA SHERIA YA BIASHARA YA ZANZIBAR NO. 4 YA 1989 NA KUWEKA VIFUNGU VYA KUIMARISHA BIASHARA ZANZIBAR NA MAMBO YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama sheria ya biashara Zanziba ,2013 itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Eneo na matumizi.

2. Sheria hii imeweka vifungu vya utawala na usimamizi wa biashara na ufanyaji wa biashara Zanzibar.

Ufafanuzi.

3. Katika sheria hii isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo.

"Mamlaka stahiki ya kutoa leseni" maana yake wizara ya serikali , idara au chombo kilichopewa uwezo na kazi za kutoa aina maalum ya leseni ya biashara.

"Wakala" maana yake ni mtu anaefanya kazi au kuongoza mambo ya msingi katika biashara ikiwa ni kwa malipo au vyenginevyo.

"Mfanyabiashara aliyeruhusiwa" maana yake ni mtu yeyote au taasisi iliyoruhusiwa kuuza bidhaa iliyokusudiwa na inajumisha mtumishi au wakala wa mtu huyo au tasisi.

"Biashara ya ziada" maana yake ni biashara inayotokana na biashara kuu au kama kampuni itashughulikia kipengele maalum cha biashara.

"Biashara" maana yake ni aina yeyote ya biashara, weledi,kazi au shughuli za biashara zinazofanywa kwa ajili ya kunufaika au kupata kipato.

"Jumuiya ya biashara" maana yake jumuiya maalum iliyosajiliwa kufanya biashara katika jamii maalum.

"Shughuli za biashara" maana yake utoaji wa bidhaa au huduma kwa kubadilishana kwa malipo.

"Kamati" maana yake ni kamati yeyote iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7 cha sheria hii.

"Jumuiya" maana yake ni Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa chini ya mkataba wa Afrika Mashariki wa 1999.

"Afisa forodha" inajumuisha mtu yeyote ukitoa kibarua aliyeajiriwa kutoa huduma za forodha kwa wakati uliopo akifanya kazi zinazohusina na forodha.

"Mahakama" maana yake ni Mahakama Kuu.

"Mkurugenzi" maana yake ni mkurugenzi wa biashara ndani ya wizara inahusiana na biashara.

“Idara” maana yake ni idara ya biashara ndani ya wizara kama ilivyoanzishwa chini ya kifungu cha 2 cha sheria hii.

“Kusafirisha bidhaa” maana yake Kutoa bidhaa sehemu yeyote ndani ya Zanzibar kwenda sehemu yeyote nje ya Zanzibar.

“Biashara ya kupitia mtandao” maana yake ni ahadi ya kuuza au kuuza bidhaa au huduma kupitia mtandao bila ya watu hao kukutana mara kwa mara.

“Bidhaa zilizopigwa marufuku kusafirishwa” maana yake ni bidhaa zilizoainishwa kuwa ni bidhaa zilizopigwa marufuku chini ya kifungu cha 42 (1) cha sheria hii

“Bidhaa zilizozuiliwa kusafirishwa” maana yake ni bidhaa zilizotangazwa kuwa zimezuiliwa kusafirishwa nje chini ya kifungu cha 42 (2) cha sheria hii.

“Gazeti” maana yake ni gazeti la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

“Bidhaa” inajumuisha aina zote ya vitu vinavyohamishika au mali ya mtu iliyoahidiwa kuuzwa au iliyouzwa inajumuisha wanyama au kiumbe hai.

“Kuingiza bidhaa” maana yake ni kuleta au kusababisha kuletwa Zanzibar kwa kupitia anga , ardhi au maji.

“Kuingiza bidhaa zilizopigwa marufuku” maana yake ni bidhaa zilizotangazwa kuwa zimepigwa marufuku kuingizwa chini ya kifungu cha 43 (1) cha sheria hii.

“Kuingiza bidhaa zilizozuiliwa” maana yake ni bidhaa zilizotangazwa kuwa ni bidhaa zilizozuiliwa kuingizwa chini ya kifungu cha 51 (2)cha sheria hii.

“Mamlaka ya utoaji leseni” maana yake ni mamlaka yeyote iliyopewa uwezowa kisheria kwa madhumuni ya kutoa leseni za biashara Zanzibar.

“Waziri” maana yake ni Waziri anaehusika na biashara.

“Wizara” maana yake ni Wizara kwa inayohusika na biashara ndani ya utawala na utekelezaji wa kazi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

“Msimamizi wa biashara” maana yake ni mtu au taasisi ambayo ndani ya eneo maalum la kiuchumi au shughuli za ujuzi akasimamia biashara ya mtaa au soko au kufanya biashara katika

eneo la shughuli za umma inajumuisha maonesho na maonesho ya biashara;

"Ruhusa" maana yake ruhusa ya kuingiza au kutoa bidhaa inayotolewa au inayochukuliwa kuwa imetolewa chini ya kifungu cha 36 (2) cha sheria hii . inajumuisha ruhusa iliyotolewa na wasimamizi wa biashara chini ya kifungu cha 35 cha Sheria hii;

"Mtu" inajumuisha ushirika, ubia, shirika, kampuni au familia;

"Pahala pa biashara" maana yake ni sehemu ya wafanya biashara kuuza huduma au bidhaa kwa jumla au rejareja na inajumuisha sehemu ya uzalishaji, hifadhi na vitu vyengine vinavyohusiana na bidhaa au huduma;

"Mamlaka ya usajili" maana yake ni mamlaka yeyote iliyopewa uwezo kisheria kwa madhumuni ya kusajili biashara Zanzibar;

"Muuzaji" maana yake ni mtu halisia ambae anawahudumia wateja kwa niaba ya mfanyabiashara au mtu ambae anauza bidhaa au anatoa huduma nje ya shughuli za kiuchumi au kiujuzi kwa njia ya mtaani au biashara ya sokoni;

"Kibali cha kuuza" maana yake nyaraka inayotolewa na msimamizi wa biashara au soko ambayo inajumuisha msingi wa kuuza bidhaa au huduma chini ya masharti yanayotolewa humu;

"SME" maana yake wafanya biashara wa kati na wadogo;

"Muangalizi" maana yake ni mtu maalum alieteuliwa kwa kuzingatia yaliyomo katika kifungu cha 18 kuwa ni muangalizi wa biashara na kufanya biashara ya bidhaa na huduma;

"Biashara" maana yake ni kuuza au kununua kwa madhumuni ya kununua inajumuisha kutoa ahadi ya kununua bidhaa au huduma;

"Mfanyabiashara" maana yake ni mtu au taasisi ambayo ndani ya eneo la shughuli za kiuchumi au ujuzi ameahidi kuuza na kuuza bidhaa au ameahidi na kutoa huduma;

"Ufanyaji biashara" maana yake ni kuingia kwenye biashara na kwa kuzingatia vifungu vyengine vya sheria, inajumuisha kutoa shughuli za kiuchumi zilizofanywa ndani ya eneo ambalo shuguli zifuatazo zinafanywa.

(a) kuuza au kuahidi kuuza bidhaa au kutoa zinazohusiana na bidhaa zilizouzwa au kutoa huduma yeyote yenye faida;

(b) kutengeneza au kufanya marekebisho ya bidhaa zilizotengenezwa kwa malipo.

(c) matengenezo au marekebisho ya bidhaa kwa malipo;

(d) kutoa huduma zilizo safi;

(e) kutoa huduma zilizofanywa vizuri;

(f) kutoa huduma ya chakula;

(g) kujumuika katika kufanya biashara sokoni;

(h) kujumuika katika kufanya biashara ya mitaani na kufanya biashara katika sehemu za wazi;

(i) na huduma nyengine yeyote inayotolewa ya madhumuni ya kufanya biashara;

(j) shughuli nyengine yeyote itakayoelezwa na Waziri.

SEHEMU YA PILI
IDARA YA BIASHARA

Kuanzishwa kwa Idara yenye majukumu ya biashara na uteuzi wa Mkurugenzi.

4.(1) Inaanzishwa idara itakayokuwa na majukumu ya uendeshaji wa biashara itakayojulikana kama idara ya usimamizi wa biashara.

(2) Kutakuwa na mkurugenzi ambae atateuliwa na Rais.

(3) Mtu hatakuwa na sifa ya kuwa mkurugenzi mpaka awe:

(a) mwenye angalau shahada ya kwanza ya chuo kikuu ya uendeshaji wa biashara au uongozi wa biashara au uchumi au sheria au utawala wa umma;

(b) awe na uzoefu wa kufanya kazi angalau wa miaka isiyopungua mitano.

Kazi za Idara.

5. Idara itakuwa na kazi zifuazo:

(a) kuishauri serikali juu ya mambo yanayohusiana na utungaji, uendelezaji, uangalizi, utekelezaji wa sera za biashara na mikakati;

(b) kusimamia sheria na sera zinazohusiana na biashara Zanzibar;

(c) kukuza soko la ndani na kimataifa;

(d) kushirikiana na taasisi nyengine katika kusimamia uuzaji wa bidhaa na kutoa huduma;

(e) kutafuta na kutoa habari za huduma za biashara zinazohusiana na uuzaji na ununuaji wa bidhaa za mlaji na bidhaa nyengine na kuishauri serikali, jumuiya za biashara pamoja na mfanyabiashara mmoja mmoja;

(f) kuendesha biashara za ndani na kimataifa na kutoa elimu na muamko mwengine wa huduma ambao ni muhimu kwa kukuza biashara;

(g) kutoa njia muafaka za kuanzisha ubia na serikali au tasisi binafsi kwenye mipango, utekelezaji na uendeshaji wa uzalishaji wa wakulima wadogo wadogo kwa bidhaa za kilimo;

(h) kukuza shughuli za biashara ndogondoga na za kati(SME) na kusisitiza kuendeleza na kupanua upatikanaji wa faida katika mapatano ya biashara ya ndani na kimataifa; na

(i) kufanya tathmini na kuusimamia mfumo wa biashara na utendaji wake;

(j) kufanya au kusababisha kufanyika kwa utafiti wa soko , kukagua na kusimamia;

(k) kukusanya, kuunganisha na kushiriki katika malipo ya biashara dhamira na maonesho ndani na nje ya nchi;

(l) kutoa utaratibu muhimu kwa wazanzibari kuweza kushiriki ipasavyo kwenye biashara za kiamataifa na maonesho ya biashara ya kimataifa;

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1) kwa maelekezo ya jumla na maalum yatakayotolewa na waziri, idara inaweza :

(a) kutoa ushauri kwa serikali , na mfanya biashara yeyote mmoja mmoja, jumuiya yeyote, taasisi kwa hatua muhimu za maendeleo kwenye mfumo wenye ufanisi kwa kufanya biashara, inajumuisha-

(i) utungaji na utekelezaji wa sera za taifa ikihusiana na matumizi ya ndani na utoaji bidhaa nje na huduma kutoka Zanzibar;

(ii) utungaji na uangalizi wa utekelezaji desturi bora za soko ikitegemea bidhaa na huduma zilizokusudiwa kwa biashara.

(b) kushirikiana na mtu mwengine yeyote, jumuiya au taasisi ndani na nje ya Zanzibar katika kuanzisha, nyenzo na uongozi wavituo vya biashara kwa kukusanya na kusambaza habari zinazohusiana na bidhaa na huduma zilizokusudiwa kwa maendeleo ya biashara;

(c) kutekeleza na kusimamia mipango, ushirikiano, jumuiya na uongozi wa maonesho ya biashara, maonesho na dhamira;

(d) kwa kushirikiana na jumuiya nyengine au taasisi, kuishauri serikali juu ya urahisishaji wa uwekaji nyaraka na kuharakisha taratibu zinazohusina na biashara; na

(e) kusaidia biashara Zanzibar kuendeleza na kupanua upatikanaji wa faida katika mapatano ya biashara ya ndani na kimataifa kwa bidhaa na huduma.

SEHEMU YA TATU
BARAZA LA USHAURI

Kuanzishwa kwa baraza

6. Kutakuwa na baraza la ushauri la biashara chini ya idara kwa ajili ya kutoa huduma za ushauri kwa ujumla katika kukuza na kuendeleza biashara Zanzibar ,

Muundo wa baraza.

7.(1) Baraza la ushauri litakuwa na wajumbe wafuatao ambao watateuliwa na waziri

(a) mwenyekiti;

(b) mjumbe ambae atateuliwa kwa kushauriana na mamlaka inayohusika kwenye taasisi zifuatazo:

(i) Wizara inayohusika na kilimo;

(ii) Wizara inayohusika na fedha;

(iii) Jumuiya ya wafanyabiashara ya taifa Zanzibar, viwanda na kilimo;

(iv) Bodi ya chakula na madawa;

(v) Wizara inayohusiana na miundombinu na mawasiliano;

(vi) Bodi ya mapato Zanzibar;

(vii) Mamlaka ya Mapato Tanzania;

(viii) Mamlaka ya serikali za mitaa Zanzibar;

(ix) Wajumbe wawili wenye ujuzi wa kutosha na uzoefu kwenye kitengo husika .

(2) Mtu hatoweza kuwa na sifa za kuwa mwenyekiti wa Baraza mpaka awe na angalau shahada ya usimamizi wa biashara, uongozi, au uchumi, au sheria au utumishi wa umma na awe na uzoefu wa angalau miaka mitano.

(3) Mkurugenzi atakuwa ni mjumbe wa kudumu wa baraza na kwa kushauriana na katibu wa Baraza ataratibu shughuli zote za baraza.

(4) Mwanasheria kutoka wizarani atateuliwa kuwa katibu wa baraza.

(5) Baraza linaweza kwa madhumuni ya utekelezaji wa kazi wenye ufanisi kuanzisha na kudumisha mfumo wenye kusaidiana kushauriana ,kushirikiana na taasisi nyengine yeyote ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na nje kwa madhumuni ya kukuza biashara Zanzibar.

(6) Baraza litachagua mmoja ya mjumbe wake kuwa makamu mwenyekiti.

Kazi za Baraza.

8.(1) Baraza litatoa huduma ya ushauri kwa ujumla kwa wizara kwenye:

(a) utungaji wa sera zinazohusiana na biashara kwa ujumla

(b) kukuza biashara na kuleta taaswira nzuri Zanzibar ikiwa kama ni kituo cha biashara

(c) kukuza soko la kimataifa na viwango;

(d) kukuza viwanda na huduma za kilimo

(e) kuanisha njia za kutatua vikwazo vya biashara Zanzibar

(f) kukuza soko la ndani

(g) afya ya jamii

(h) shughuli nyengine yeyote ambayo litapangiwa na Waziri au Katibu Mkuu wa Wizara

Mkutano wa baraza.

9.(1) Baraza kawaida litakuwa linakutana kwa ajili ya kazi zake za kawaida wakati na pahala litapoona linafaa, lakini kwa namna yeyote ile litakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu;

(2) Mkurugenzi , mwenyekiti na ikiwa mwenyekiti hayupo basi makamu mwenyekiti anaweza wakati wowote kuitisha mkutano wa dharura wa baraza pale ambapo kuna ombi la maandishi kwa wajumbe walio wengi wa baraza ndani ya Ofisi;

(3) Mwenyekiti na ikiwa mwenyekiti hayupo basi makamu mwenyekiti anaweza na pale ambapo kuna ombi la wajumbe walio wengi kumualika kwenye mkutano mtu yeyote ambae si mjumbe kushiriki katika jambo lililokusudiwa na baraza lakini mtu huyo hatostahiki kupiga kura.

(4) Akidi ya kila mkutano wa Baraza itakuwa nusu ya wajumbe , na maamuzi yatakuwa wingi wa kura na ikitokea kuwa na kura zilizofungana basi mwenye kiti atakua na kura ya ziada ambayo ni nyongeza ya kura ya mwanzo.

(5) Katibu ataweka kumbukumbu na ataweka kwa kina mambo yote yaliyofanyika au kukubaliwa na baraza katika mkutano unaostahiki.

(6) Kumbukumbu za kila mkutano wa baraza zitathibitishwa na kusainiwa katika mkutano unaofuata wa baraza na wote Mwenyekiti na Katibu.

10. Baraza litapokea fedha zake kutoka kwenye idara inayohusika. fedha za baraza .

11.(1) Baraza kila baada ya miezi mitatu baada ya kufungwa mwaka wa fedha litaandaa na kuwasilisha kwa waziri kupitia kwenye idara taarifa ya shughuli, utendaji na maamuzi yaliyochukuliwa na baraza ndani ya mwaka wa fedha unaohusika. Taarifa ya mwaka.

SEHEMU YA NNE
MAMALAKA YA USIMAMIZI

12. (1) Idara itakuwa na mamlaka ya ujumla ya usimamizi katika kutilia nguvu sheria hii. Mamalaka ya usimamizi.

(2) Mamlaka zifuatazo kwa kusaidiana na idara na bila ya kuathiri masharti ya sheria hii na sheria zilizoanzisha mamlaka hizo kuwateuwa watu maalum ndani ya mipaka ya uwezo wao kufanya kazi ya usimamizi juu ya kushikamana na sheria hii na mahitaji mengine yaliyoanzishwa katika msingi huo, mamlaka hizo ni hizi zifuatazo:

(a) Taasisi ya kumlinda mtumiaji na usawa katika kufanya biashara;

(b) Bodi ya madawa na chakula;

(c) Taasisi ya mizani na vipimo;

(d) Bodi ya mapato Zanzibar;

(e) Malmlaka ya mapato Tanzania;

(e) Shirika la Viwango Zanzibar;

(f) Mamlaka inayohusiana na utoaji wa leseni;

(g) Baraza la manispa, Miji na Halmashauri za Wilaya;

(i) na taasisi nyengine yeyote ambayo imepewa mamlaka kisheria yenye kufanya kazi za biashara na kusimamia biashara.

(3) Kila moja ya tasisisi yenye mamlaka ya usimamizi iliyoainishwa katika kifungi kidogo cha kwanza cha kifungu hiki atateuwa idadi ya kutosha ya watu maaalum wawe wasimamizi wa biashara na kufanya biashara ya bidhaa na huduma.

(4) Kila msimamizi ambae anafanya kazi ya usimamizi chini ya masharti ya Sheria hii atatoa kitambulisho ili kuthibitisha mamlaka ya usimamizi anayoifanyia kazi.

13. Pamoja na uwezo waliokuwa nao chini ya kifungu cha 18 cha Sheria hii na chini ya Sheria nyengine yeyote kila msimamizi atakuwa na uwezo wa ziada ufuatao. Uwezo wa wasima-mizi.

(a) kusimamia utiifu wa sheria hii bila ya vikwazo vya aina yeyote

(b) kuingia bila ya kuekewa kikwazo chochote eneo au jengo linalotumiwa na muuzaji, mfanyabiashara au msimamizi wa

biashara au chombo kilichochukuwa bidhaa za mfanyabiashara, au kujua njia za usafiri zinazotumiwa na mfanyabiashara, msimamizi wa biashara, wawakilishi wao au waangalizi waadilifu;

(c) kupata habari ambazo ni muhimu kwa ajili ya kufanya kazi za wasimamizi kutoka kwa wauzaji wanaohusika, wafanyabiashara, wasimamizi wa biashara au taasisi zilizopewa mamlaka na Serikali;

(d) kuchunguza bidhaa na huduma zilizouzwa au kutarajia kuuza pamoja na nyaraka zinazohusiana na bidhaa hizo na huduma na kupata vivuli hivyo;

(e) kuzuia nyaraka zilizoambatana na bidhaa zilizouzwa au huduma zilizotolewa;

(f) kukagua uwiano wa bidhaa au huduma, kuuzwa kwa bidhaa au huduma na pahala pa biashara panapohitajika kulikowekwa chini ya mashariti ya Sheria hii;

(g) kutoa miongozo;

(h) kuwashurutisha wafanyabiashara kuijulisha jamii juu ya hatari yeyote inayohusiana na bidhaa inayouzwa au huduma inayotolewa;

(i) kuthibitisha uhalali na usahihi wa nyaraka yeyote inayothibitisha haki ya kuuza bidhaa au huduma ikiwa shurti ya kuzuia nyaraka hiyo imetolewa na Sheria;

(j) kuthibitisha uhalali na usahihi wa usajili ikiwa kuna mambo ya kuzingatia ya usajili yameelezwa na Sheria;

(k) bila ya kuathiri mashariti ya kifungu kidogo cha (2) wasimamizi watakuwa na wajibu wa kuchukuwa sampuli ya bidhaa au bidhaa ya huduma iliyotolewa kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

(2) Mamlaka ya usimamizi itabeba gharama zote za huduma za tathmini ambazo zinatokana na uchunguzi wa bidhaa na huduma na atarejesha bidhaa au ikiwa mfanya biashara atakubali, kumfidia mfanyabiashara kwa thamani ya bidhaa au huduma ikiwa kutokana na maoni ya mtaalam bidhaa na huduma zimekidhi mahitaji yaliyoelezwa ikiwa

(a) kutokana na maoni ya mtaalamu bidhaa au huduma ambazo hazikufika kiwango vya gharama za huduma ya tathmini basi zitalipwa na mfanyabiashara; na

(b) bidhaa au huduma ambazo hazikufika viwango hazitorejeshwa wala kufidiwa.

(3) Katika kutekeleza majukumu yao, wasimamizi watazingatia siri za biashara na taarifa za kiufundi ambazo zitajulikana kwao katika

kutekeleza kazi zao za usimamizi isipokuwa kutoa habari hiyo imeruhusiwa na Sheria .

Amri kutoka kwa wasima-mizi.

14. (1)Msimamizi anaweza kutoa amri ambazo zitawafunga wauzaji na wafanyabiashara na wapangaji wa biashara ikiwa;

(a) mfanyabiashara au muuzaji anajishughulisha na bidhaa au huduma ambazo hazikufikia viwango;

(b) mfanyabiashara anauza bidhaa bila ya kuwa na nyaraka zinazohitajika;

(c) sehemu anayoifanyia biashara haikufikia kiwango kinachokubalika;

(d) mfanya biashara anafanya biashara bila ya nyaraka zinazothibitisha haki ya kuuza bidhaa au huduma, ikiwa imehitajika na sheria kwamba nyaraka hizo ziwepo; au

(e) mfanyabiashara au msimamizi wa biashara ambae anafanya biashara bila ya usajili au bila ya makubaliano ya maandishi ya usajili kama inavyatakiwa kisheria.

(2) Katika kutoa amri chini ya mashariti ya kifungu kidogo cha (1) mtu maalum atafanya yafuatayo katika kutekeleza kazi za usimamizi

(a) kumjuilisha muuzaji, mfanyabiashara au msimamizi wa biashara vyovyote vile itakavyokuwa juu ya makosa yaliyofanywa na kutaka mauzo hayo au ahadi ya kuuza bidhaa au huduma kughairishwa au bidhaa au huduma ziondolewe kwenye kuuzwa; au

(b) kuelekeza kwamba hatua muhimu za kisheria za kuendeleza uuzaji wa bidhaa au huduma zilizoharibika;

(3) Muuzaji yeyote, mfanyabiashara au msimamizi wa biashara ambae atashindwa kukubaliana na amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na endapo akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili (200,000/=).

SEHEMU YA TANO
USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

Usajili wa biashara

15. (1) Kutakuwa na wasajili wafuatao wa kudumu kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi za biashara;

(a) Msajili wa wafanya biashara na biashara ambazo zitaekwa na kudumishwa chini ya Sheria inayohusika na usajili wa biashara;

(b) Msajili wa wasimamizi wa biashara katika soko la muda na matukio ya umma ambayo yataekwa na Manispaa, Miji na halimashauri za Wilaya;

(c) Msajili wa viwanda, ndege, vyombo vya moto na vyombo vya baharini ambavyo vitashughulikiwa na mamlaka husika za utoaji leseni kwa namna yeyote iliyoelezwa kisheria;

(2) kumbukumbu zilizowekwa chini ya kifungu kidogo cha (1) ya kifungu hiki zitasambazwa katika Tasisi tofauti kwa malengo ya uendeshaji mzuri wa biashara

Utoaji leseni za biashara.

16. Kila mtu au wakala anaefanya biashara atakuwa na leseni iliyotolewa na mamlaka ya leseni inayotambulika baada ya kutekeleza masharti kama yalivyoelezwa chini ya sheria inayohusika

Mipaka ya mamlaka ya leseni ya biashara.

17. (1) Leseni ya biashara itamruhusu mtu aliepewa kufanya biashara katika eneo lililoanishwa ndani ya leseni hiyo na hii itachukuliwa pia ruhusa kwa mwenye kibali hicho kuendesha biashara nyengine ya ziada katika eneo hilo.

Isipokuwa kwamba:

(a) kwa leseni ya biashara ya uendeshaji wa benki au uendeshaji wa meli na vyombo vya baharini itachukuliwa kuwa haikumruhusu mtu aliepewa kufanya biashara yeyote ya ziada;

(b) hakuna mtu ataeruhusiwa kufanya biashara zilizotajwa katika aya ndogo ya (a) katika kifungu hiki isipokuwa awe ameruhsiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa leseni iliyotolewa inayohusiana na biashara hiyo;

(c) hakuna leseni itakayotolewa na Sheria inayohusika ambayo itachukuliwa kuruhusu kufanyika kwa biashara kama biashara ya ziada, ya biashara yeyote ambayo inaweza kuwa halali kuendeshwa ikiwa leseni, kibali au mamlaka nyengine imetowa au chini ya Sheria nyengine yeyote;

(d) hakuna malipo ya leseni ya biashara ambapo patahitajika kufanyika tathmini ya mwaka na kurejesha taarfa inaweza kuendeshwa kama biashara ya ziada chini ya leseni ya biashara ambapo malipo ya leseni hayatohitajika kufanyiwa tathmini;

(e) hakuna biashara ambayo kiwango cha malipo ya leseni kilichoainishwa kimelipwa inaweza kuendesha kwa njia ya rejareja au kama biashara ya ziada chini ya malipo ya leseni ambayo yanahitaji kufanyiwa tathimini ya mwaka na kutoa marejesho;

(f) hakuna mtu chini ya mamlaka yeyote ya leseni ya biashara ambae ataendesha biashara yeyote ya ziada kinyume na leseni yake ambayo imetolewa na Halimashauri ya mitaa;

(g) hakuna leseni ambayo itatolewa chini ya Sheria yeyote inayohusika itakuwa na athari ya kumruhusu mtu yeyote kuendesha aina yeyote ya biashara iliyopigwa marufuku na Sheria nyengine yeyote Zanzibar au kutoa msamaha kwa mtu yeyote kutofungamana na masharti yeyote, mipaka au mahitaji mengine yaliyowekwa au yaliyoelezwa na Sheria nyengine yeyote inayohusiana na biashara hiyo;

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki biashara ya ziada maana yake ni biashara.

(a) ambayo siyo iliyoainishwa katika leseni iliyotolewa na;

(b) ambapo ;ikiwa leseni tofauti zimetumika kwa biashara hiyo malipo ya leseni yaliyolipwa kwa leseni hiyo hayatozidi malipo ya leseni kwa leseni iliyotolewa;

(3) Ambapo ,kuhusiana na leseni yeyote iliyotolewa chini ya kifungu hiki biashara yeyote ambayo ilikuwa biashara ya ziada katika wakati ambao leseni hiyo imetolewa, biashara hiyo itaendelea na itachukuliwa kuwa ni biashara ya ziada kwa mujibu wa leseni hiyo kwa kipindi chote cha uhalali wa leseni, bila ya kuathiri ongezeko la malipo ya leseni kwa leseni ya biashara kwa kuendesha biashara hiyo ya ziada;

Maombi ya usajili na leseni.

18.(1) Mtu yeyote ambae anataka kuingia kwenye biashara au kusimamia biashara anaweza kuomba biashara yake isajiliwe au ipate leseni kwa kujaza na kuwasilisha kwenye mamalaka husika ya usajili au utoaji leseni fomu iliyo na maelezo kutoka kwa mamalaka ya usajili au leseni.

(2) Ikiwa maombi yaliyowasilishwa ni ya kuuza bidhaa au kutoa huduma katika vyombo vya majini au vya angani ambavyo vinatumika kutoa huduma kwa abiria alama inayokitambulisha chombo (namba ya usajili) itawekwa kwenye maombi kuwa ni sehemu ya biashara.

(3) Ikiwa maombi ni ya biashara ya kusimamia katika sehemu za wazi fomu ya maombi ioneshe jina, wakati na pahala panapokusudiwa kufanywa biashara.

(4) Ikiwa maombi ni ya kufanya biashara kwa msimu eneo ambalo mfanyabiashara anatarajia kuuza bidhaa au kutoa huduma lazima lioneshwe kwenye fomu yake ya maombi.

(5) Ikiwa maombi yaliyowasilishwa ni ya kuuza bidhaa au kutoa huduma bila ya kuwa na sehemu maalum ya kufanyia biashara neno"bila ya kutokuwa na sehemu maalum " litajazwa kwenye sehemu ya fomu ya maombi yakuendesha biashara hiyo.

(6) Ikiwa muombaji anatarajia kuuza bidhaa au kutoa huduma nje ya eneo ambalo ameruhusiwa kufanya biashara neno" nje ya eneo la biashara aliloruhusiwa " litaoneshwa kwenye fomu ya maombi ya kuendeshea biashara hiyo.

(7) Ikiwa muombaji anatarajia kuuza bidhaa au kutoa huduma kwa njia ya mtandao atapaswa kuandika anuani kamili namna anavyoweza kupatikana katika mtandao huo na namna anavyoweza kutoa huduma.

(8) Ikiwa muombaji anatarajia kufanya biashara ya kusimamia biashara katika eneo la wazi msimamizi huyo wa biashara atapaswa kuanisha eneo hilo la wazi ambalo biashara hiyo inakusudiwa kufanywa.

Kazi za mamlaka ya utoaji wa leseni

19. Pamoja na kazi walizopewa juu mamlaka ya utoaji leseni chini ya mashariti ya Sheria nyengine yeyote mamlaka ya leseni itakuwa na kazi zifuatazo za ziada.

(a) kutoa leseni baada ya kujiridhisha kwamba masharti muhimu yametekelezwa kwa mfanyabiashara kuwa na leseni inayomruhusu yenye kufanya aina hiyo ya biashara iliyokusudiwa;

(b) baaada ya kwisha kutolewa leseni mamlaka itapaswa kutoa masharti muhimu kwa mfanyabiashara ambae atapaswa ayazingatie katika uendeshaji wa biashara ya aina hiyo;

(c) kila itakapowezekana ,mamalaka itafanya ukaguzi wa eneo ambalo biashara inafanyika na ijiridhishe kwamba eneo la biashara na kuanzishwa kwake limekidhi mahitaji yaliyoelezwa au ni muhimu kwa uendeshaji mzuri kwa aina hiyo ya biashara inayohusika.

SEHEMU YA SITA
UUZAJI WA BAADHI YA BIDHAA NA UTOAJI HUDUMA

Uuzaji wa baadhi ya bidhaa.

20. (1) Waziri anaweza baada ya kushauriana na mamlaka zinzohusika, kudhibiti uuzaji wa bidhaa yeyote au huduma kwa maslahi ya umma kwa:-

(a) kupiga marufuku uuzaji wa bidhaa yeyote katika eneo maalum au kwa aina yeyote ya bidhaa ya mfanyabiashara , au taasisi ya umma kama ilivyoanishwa katika amri; au

(b) kupanga aina yeyote ya bidhaa kuwa ni bidhaa ambayo inaweza kuuzwa tu na mfanyabiashara aliepewa mamlaka kama ilivyoainishwa katika amri.

(2) Ikiwa Waziri ametoa amri chini ya kifungu hiki, hakuna mtu mwengine zaidi ya mfanyabiashara aliepewa mamlaka ndie ataeuuza, ahadi ya kuuza au kuonesha katika sehemu yake bidhaa alizopanga au vyovyote itavyokuwa hakuna mtu atakaeuza, kutoa ahadi ya kuuza au kuonesha bidhaa yeyote katika eneo ambapo uuzaji wa bidhaa hizi umepigwa marufuku.

(3) Mtu yeyote ambae ataenda kinyume na masharti ya kifungu hiki itakuwa ametenda kosa na endapo akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua laki moja (1000,000/=) au kifungo cha kipindi kisichozidi miezi mitatu au vyote viwili faini na kifungo, kwa kuongezea mahakama inawea kutoa amri kuwa bidhaa zinazohusika zitaifishwe.

Wajibu wa mfanyabia shara.

21.(1) Kila mfanya biashara Zanzibar atapaswa kuzingatia mambo yafuatayo.

(a) atafuata Sheria na kanuni zinazoongoza biashara iliyoanzishwa, kusajiliwa na kupata leseni;

(b) kuridhika na mahitaji yanayoongoza uuzaji au ahadi ya kuuza bidhaa au huduma kama ilivyoelezwa na leseni ya biashara inayohusika;

(c) kuhakikisha kwamba bidhaa na huduma zinazouzwa au zinazotarajiwa kuuzwa zipo kwenye viwango na hivyo inafaa kwa kuuza na matumizi;

(d) kuthibitisha,wakati anapokea bidhaa kwamba zinakubaliana na nyaraka zake zilizoambatanishwa, nyaraka hizo zieleze viambatisho, kiwango na ubora wa bidhaa iliyopokelewa na kwamba bidhaa imekidhi viwango vinavyohitajika kwa matumizi;

(e) kuhakikisha kwamba njia au vifaa vinavyotumika kufanyia vipimo vipo sawa kwa biashara huska iliyoanzishwa na vipo sahihi;

(f) kuruhusu na kuwasilisha kwa upekuzi na kutoa vivuli , kwa mtu ambae anafanya kazi ya usimamizi hapo nyaraka zote zinazohusina na usajili wa biashara, leseni, nyaraka zake zilizoambatanishwa na bidhaa na nyaraka zinazothibitisha kukubaliana na viwango vya bidhaa zilizouzwa nakutoa huduma au zinazotarajiwa kuuzwa;

(g) kutoa mafunzo kwa watendaji wake na utaalamu muhimu kwa ajili ya utendaji mzuri wa kazi;

(h) kuonesha alama kwenye sehemu yenye kuonekana wazi wazi mbele ya sehemu ambayo biashara inafanyika, inayoonesha pamoja na mambo mengine jina la biashara na anuani ya mfanyabiashara, bidhaa au huduma inayouzwa , namna ya kuuzwa ikiwa ni njia ya jumla au reja reja, muda wa kawaida wa kufungua na kufunga biashara na taarifa nyengine yeyote yenye maslahi kwa mfanyabiashara;

(i) pale biashara itakaposimama au kumalizika atoe taarifa ya kusimama na kumalizika kwa shughuli zake za biashara;

(j) kutoa beji ya utambulisho kwa watendaji wake na kuhakikisha wanazivaa wakati wote wa kazi;

(k) kubainisha, wakati wa uuzaji wa bidhaa au kutoa huduma kupitia mtandao jina la biashara la mfanyabiashara, maelezo ya bishara ya mfanyabiashara , mfumo wake wa kufanya biashara na baadhi ya habari nyengine kwa maslahi ya mfanyabiashara;

(l) pale malipo ya bidhaa au huduma yanapofanyika kwa kutumia kadi ya mtandao *(e-card)* atoe utaratibu unaotumika kwa kadi hiyo mbele ya mnunuzi au mteja na kutoa taarifa za ziada kwa ajili mnunuzi au mteja;

(m) kuzingatia usafi wa mazingira na afya unaohitajika katika eneo na mazingira jirani ya biashara.

(2) Bila ya kuathiri Sheria nyengine yeyote inayofanya kazi Zanzibar ni marufuku kufanya biashara ya:

(a) kuzuia upatikanaji wa haki kuzuia kufanya upendeleo wa kuuza au kutoa ahadi ya kuuza bidhaa au huduma au biashara ya kuwashawishi wateja kwa kuzishushia hadhi bidhaa au huduma ya mfanyabiashara mwengine au kupiga marufuku matumizi ya majina ya biashara au kwa namna nyengine yeyote ambayo ni kinyume na maadili mazuri ya biashara, au desturi za ufanyaji biashara;

(b) kukubali au kutoa ahadi ya kuuza bidhaa au huduma uendeshaji wake au utaratibu wake umekatazwa kwa mujibu Sheria; au

(c) kukubali kununua bidhaa kutoka kwa mtu ambae hana haki ya kuuza au kuishughulikia bidhaa kwa namna ambayo kwamba bidhaa au shughuli hiyo imedhibitiwa kwa mujibu Sheria.

Kazi za wasimamizi wa biashara.

22. Kila msimamizi wa biashara atakua na kazi zifuatazo:

(a) ahakikishe kwamba sehemu ya biashara imekidhi mahitaji kama yalivyoainishwa katika utaratibu wa uuzaji bidhaa au utoaji ambao umeruhusiwa katika sehemu hiyo;

(b) kuhakikisha kwamba bidhaa au huduma zinatolewa katika sehemu ya uuzaji na katika wakati wa biashara ulioelezwa kwa madhumuni hayo; na

(c) kutoa risiti na kibali cha kuuza bidhaa au utoaji huduma kwa kuzingatia vigezo vya Sheria hii.

Kazi za muuzaji.

23.(1) Kila muuzaji au anaekusudia kuuza bidhaa au kutoa huduma kwa mtu yeyote anaetoa huduma kwa wateja kwa niaba ya muuzaji au anaekusudia kuuza awe na mambo yafuatayo:

(a) awe na taaluma yakutosha juu ya bidhaa au huduma inayotolewa;

(b) popote atakapohitajika, atoe taarifa sahihi zinazohusiana na sifa, asili,masharti ya matumizi, bei na uhakika wa kubadili bidhaa na dhidi ya bidhaa zenye kasoro na huduma itolewayo na kusudio la matumizi ya kimataifa au kutambulika kwa ishara kwa ujumla kwa maombi ya mteja ;

(c) wakati wa kuuza bidhaa au kutoa ,huduma nje ya sehemu ya biashara ya mfanyabiashara, iliyothibitishwa, kupitia maombi ya mteja au wasimamizi makhususi, uwezo wake wa kuhudumia wateja kwa niaba ya mfanyabiashara

(d) ikiwa uuzaji au ahadi ya uuzaji unafanywa Mitaani, Sokoni au kwenye sehemu ya wazi avae tagi yenye jina ambayo itarahisisha utambulisho wake; na

(e) kwenye uuzaji wa bidhaa au huduma ambazo ingawa zimekubaliana na mahitaji ya kisheria, zipo chini ya kiwango cha kawaida au bidhaa zilizotumika, taarifa za athari hiyo zitaoneshwa katika sehemu ya uuzaji wa bidhaa au utoaji wa huduma .

Mambo ya kuzingatia katika uuzaji wa bidhaa na utoaji huduma.

24.(1) Uuzaji wa bidhaa utakubaliana na mahitaji yaliyoanzishwa ya uuzaji wa bidhaa kwa kuzingatia vifungu vya Sheria vinayohusiana na uuzaji wa bidhaa chini ya sehemu ya saba ya Sheria ya Mikataba na vifungu vya Sheria nyengine yeyote inayohusika yenye kufanya kazi Zanzibar.

(2) Ambapo uuzaji umefanyika bila ya kuendana na mahitaji yanayohitajika kisheria na kwenye uuzaji wa bidhaa ambazo zimeshatumika, taarifa ya athari hii itaoneshwa katika sehemu ya uuzaji wa bidhaa hizo.

(3) Uuzaji wa bidhaa utaendana na mahitaji yaliyoanzishwa kwa uuzaji wa bidhaa au utoaji huduma hiyo kutokana na Sheria inayohusika.

(4) Ambapo uuzaji wa bidhaa au huduma unafanywa nje ya eneo ambalo mauzo ya ujumla, rejareja, utoaji wa huduma iliyoanzishwa nje ya sehemu ya uuzaji, mfanya biashara atalazimika kuweka jina la biashara au jina na mambo ya msingi ya Mkataba wa mfanyabiashara, jina na bei ya bidhaa na huduma kutoka kwa mteja

(5) Ikiwa kazi ya kutekeleza amri itekelezwe bila ya kuwepo wateja, mfanya biashara atatoa nyaraka au kuweka alama kwa mteja ambayo inathibitisha upokeaji wa amri.

(6) Uwekaji wa alama uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha hapo juu utawezeshwa kumtambulisha mfanyabiashara kwa majina ya biashara, jina au namba ya usajili.

(7) Ikiwa amri imetekelezwa mbele ya mteja nyaraka inayothibitisha upokeaji wa amri itatolewa kwa mteja kwa maombi ya mteja.

Kufanya biashara za mtaani.

25.(1) Kila mtu ambae anauza bidhaa au anatoa huduma nje ya shughuli za kiuchumi kwa njia za kusambaza mitaani au kufanya biashara sokoni au katika sehemu za wazi atapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) awe na ujuzi au taaluma wa bidhaa na utoaji huduma anayouza

(b) kushikamana na mahitaji yaliyoanzishwa kwa kuuza bidhaa au utoaji wa huduma

(c) kuvaa kitambulisho chenye jina lake na kilichowekwa kwenye sehemu inayoonekana

(2) Kwa madhumuni yaliyomo kwenye kifungu kidogo cha (1) upanuzi wa sehemu ya muuzaji nje ya huduma zake za uuzaji wa eneo lake la haitachukuliwa kuwa ni biashara ya mtaani.

(3) Pamoja na vifungu vya Sheria hii, Manispaa, Miji, na Halimashauri za Wilaya wanaweza kutoa taratibu nyengine za masharti kwa biashara ya mtaani au kufanya biashara Sokoni na kwenye mgongano kati vifungu vya Sheria hii na Kanuni za Mamlaka hizi, Sheria hii ndio itakayokuwa na nguvu.

Ufanyaji biashara sokoni.

26.(1) Katika kufanya biashara Masokoni, muuzaji au mfanya biashara atauza bidhaa au kutoa huduma au kufanya biashara kwa mujibu wa ruhusa aliyopewa na msimamizi wa Soko, ambayo imeainisha pamoja na mambo mengine pahala, muda, na namna ya biashara itakavyoendeshwa

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1) ni marufuku kuuza bidhaa zozoote ambazo zilizopigwa marufuku kisheria kuuzwa Sokoni.

(3) Katika ufanyaji biashara Sokoni, bidhaa zilizotumika, wanyama ndani ya tafrsiri ya Sheria ya Uongozaji rasilimali wanyama na mimea itauzwa katika sehemu tofauti, soko maalum kwa ajili ya kuuzia kundi hili la bidhaa, wanyama na mimea kama vyovyote vile inaweza kuwa.

Kufanya biashara kwenye sehemu za wazi

27.(1) Muuzaji yeyote au mfanyabiashara wa bidhaa au mtoa huduma anaweza kuuza au kutoa huduma kwenye sehemu ya wazi kwa uuzaji kilichotolewa na msimamizi wa biashara hiyo.

(2) Pamoja na masharti yaliyomo katika vifungu vya Sheria hii, Manispaa, Miji na Halimashauri za Wilaya vyovyote vile itakavyokuwa inaweza kwa amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali,kutoa utaratibu na masharti ya ziada ya yatakayosimamia uuzaji au kufanya biashara katika sehemu za wazi.

Mambo ya kuzingatia katika utoaji vibali vya uuzaji.

28. Kibali cha kuuza au kufanyia biashara kilichotolewa na masharti ya kifungu cha 27 (1) cha Sheria hii kitaweka mambo yafuatao.

(a) Jina, pahala na namba ya usajili ya msimamizi wa biashara;

(b) Jina na namba ya usajili ya mfanyabiashara namba ya mawasiliano ya msajili, na pahali pa biashara;

(c) Namba ya kibali cha kufanya biashaa;

(d) Eneo la pahala pa kufanyia biashara;

(e) Orodha ya bidhaa na huduma zinazouzwa katika eneo la biashara;

(f) Muda wa kufanya biashara;

(g) Muda wa kibali cha kufanyia biashara;

(h) Bei ya kibali cha kufanyia biashara.

Upunguzaji wa bei wa bidhaa.

29.(1) Maneno yote yanayotumika kumaanisha punguzo la bei au maneno mengine na maelezo yenye maana sawa yanaweza kutumika kutoa taarifa kuhusu uuzaji wa bidhaa za punguzo ikiwa:

(a) Bidhaa zote zinazouzwa au mipaka ya uchaguzi wa bidhaa kiwekwe kwenye punguzo la bei;

(b) Uuzaji ni wa muda maalum;

(c) Bei ya bidhaa zinazouzwa chini ya masharti, kama hayo huwa ipo chini kuliko bei ya kawaida.

(2) Neno kuuza, punguzo au maneno mengine au maelezo mengine yenye maana sawa yanaweza kutumika kutoa habari za pungzo la bidhaa ikiwa:

(a) ni bidhaa kawaida huuzwa na mfanyabiashara ambayo inauzwa kwa punguzo;

(b) uuzaji ni wa kipindi maalum;

(c) bei ya bidhaa inayouzwa chini ya masharti hayo ipo chini kuliko bei ya kawaida.

SEHEMU YA SABA
UDHIBITI WA UIGIZAJI NA USAFIRASHAJI BIDHAA

Bidhaa zenye kudhibi-tiwa..

30.(1) Waziri anaweza kwa amri iliyochapishwa ndani ya Gazeti la Serikali kutangaza bidhaa zenye kudhibitiwa uingiaji au usafirishaji wake pamoja na kutoa sababu ya kufanya hivyo

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki cha Sheria hii, itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote mwenye kuingiza au kusafirisha bidhaa yeyote inayodhibitiwa au kufanya jambo lolote kwa dhamira ya kuingiza bidhaa zenye kudhibitiwa isipokuwa pale ambapo atakuwa na kibali kilichotolewa na waziri kinachohalalisha uingizaji au usafirishaji wa bidhaa hizo

(3) Waziri hatotoa kibali cha uingizaji wa bidhaa yeyote yenye kudhibitiwa ikiwa uingizaji wa bidhaa hizo utahatarisha makubaliano au mpangilio wowote wenye kuhusiana na biashara za ndani au za Kimataifa zilizoingiwa au kukubaliwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano au Serikali ya mapinduzi Zanzibar

(4) Waziri atatoa kibali chini ya kifungu kidogo cha 2 bila ya kuathiri masharti yatakayoelezwa na kanuni

(5) Waziri anaweza baada ya kupata uhakika wa kukataa kutoa kibali cha usafirishaji wa bidhaa kwa mfanyabiashara alieomba, isipokuwa Waziri akiridhika kuwa mfanyabiashara huyo amezipata bidhaa zake kihalali kutoka kwa mzalishaji;

(6) bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), aina za zifuatazo zinaweza kuingizwa bila ya leseni yeyote ikiwa bidhaa hizo zenye kudhibitiwa au vyenginevyo:

(a) bidhaa zenye kupita njia wakati wa usafirishwaji;

(b) mzigo unaoaminika kama ilivyofafanuliwa na Sheria ya Forodha au Sheria inayorekebisha Sheria yoyote inayotumika Zanzibar;

(c) mizigo ya kibalozi, kijeshi na vifaa vya wanamaji kama ilivyofafanuliwa na Sheria ya Forodha;

(d) bidhaa za mfano za mfanyabiashara;

(e) bidhaa zilizotumwa kwa posta baada ya Mkurugenzi kuridhika kuwa ni zawadi iliyokuwa haikuombwa na ambayo haikusudii kuuzwa;

(f) bidhaa zilizoagizwa na Serikali ya Mapidnuzi Zanzibar.

(7) Bila ya kuathiri kifungu chengine chochote cha Sheria hii, hakuna kibali kitakachotolewa chenye kuhusina na usafirishaji wa bidhaa zifuatazo:

(a) bidhaa ambazo ni sehemu ya bidhaa za kawaida

(b) bidhaa zilizoingizwa katika mzigo ambao kwa Zanzibar umepitishwa tu kwa nyaraka za usafirishaji chini ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki au Sheria nyengine yoyote ya Afrika Mashariki au Kanuni chini ya Sheria hizo;

(c) bidhaa zinazotumika kama bidhaa binafsi vilivyochukuliwa na msafiri au zilizoagizwa na msafiri huyo au kwa niaba yake ndani ya muda usiozidi miezi sita tokea tarehe ya kuondoka kwake Zanzibar;

(d) bidhaa iliyoagizwa kama za mfano wa biashara;

(e) bidhaa ambazo ni za chakula ambazo ni sehemu za mzigo wa msafiri halali;

(f) bidhaa ambazo ni zawadi ambazo hazikuombwa na ambazo zimeingizwa kwa njia ya posta.

(8) Waziri anaweza kwa amri iliyochapishwa ndani ya gazeti la serikali kuzuia aina, kiasi,idadi, au thamani ya bidhaa ambazo zinazoweza kusafirishwa bila ya leseni ya usafirishaji chini ya kifungu kidogo cha 7 (e) au(f)

Ombi la kupewa kibali cha uingizaji au usafirishaji bidhaa.

31. Maombi ya kupewa kibali cha uingizaji au usafirishaji wa bidhaa au huduma nyengine yeyote yatafanywa kwa wizara husika.

Utoaji wa kibali.

32.(1) Bila ya kuathiri kifungu chengine chochote cha Sheria hii Waziri anaweza kutoa kibali kwa amri ya kisheria kwa mtu yeyote kwa kuingiza au kusafirisha bidhaa zenye kudhibitiwa au aina nyengine yeyote ya bidhaa zilizoainishwa kwenye amri kwa kuwekewa masharti kama akihisi inafaa kufanya hiyvo.

(2) Bila kuathiri mambo ya ujumla yaliyotangulia, Waziri anaweza kutoa masharti yote au sehemu ya masharti yenye kuhusiana na bidhaa zilizoruhusiwa kuingizwa au kusafirishwa ziwe .

(a) zimewekwa kwenye mahali pakufikia kama ilivyoainishwa kwenye kibali cha ujumla;

(b) isipindukie idadi au thamani iliyoainishwa kwenye kibali cha ujumla kwa mzigo;

(c) bidhaa ziwe zimesafirishwa au kuingizwa katika hali yeyote ile ikiwa kupitia bandarini au kwa njia nyengine ya utoaji iliyoeleza kwenye kibali cha ujumla.

Utoaji wa kibali cha uingizaji na usfirishaji wa bidhaa au huduma nyengne yeyote.

33.(1) Bila ya kuathiri kifungu cha Sheria hii Waziri kwa kupata maombi ya utoaji wa kibali cha kusafirisha au kuingiza bidhaa au huduma nyengine yeyote kitatolewa kwa mujibu wa masharti yafuatayo:

(a) kimetolewa kwa kusafirisha au kuingiza bidhaa kwa muda maalum na kikawekewa masharti ikiwa yapo; au

(b) kukataa kutoa kibali cha kusafirisha au kuingiza bidhaa.

(2) Kibali cha kuingizia au kusafirishia bidhaa kitatolewa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa ndani ya Kanuni ya Sheria hii.

Utenguaji wa kibali.

34.(1) Waziri atatengua kibali cha kuingiza au kusarifisha bidhaa ikiwa:

(a) muombaji amevunja masharti kama yalivyoainishwa kwenye kibali hicho au kanuni;

(b) muombaji ameshindwa kuendana na masharti ya kibali hicho;

(c) kibali kimepatikana kwa njia ya udanganyifu au uwasilishaji mbaya.

(2) Waziri anaweza wakati wowote kutengua kibali chochote cha usafirishaji kwa usafirishaji wa vyakula vya aina yeyote ikiwa ataridhika ya kwamba kuna uhaba au uhaba unaotarajiwa kutokea wa vyakula ndani ya Zanzibar.

Uwezo wa Waziri wa kupiga marufuku au kuweka mipaka ya uingizaji au usafirishaji wa bidhaa.

35.(1) Bila ya kuathiri kifungu chengine chochote cha Sheria hii, Waziri anaweza kwa amri iliyochapishwa ndani ya Gazeti la Serikali, kupiga marufuku moja kwa moja, kuzuia au kurudisha au kupinduwa kwa mtu yeyote, au kuweka mipaka ya uingizaji au usafirishaji wa bidhaa wa aina yeyote kutoka au kwenda nchi yeyote kama itakavyoainishwa na amri hiyo,

ikiwa kitendo hicho kwa maslahi ya Zanzibar na ikiwa hayiendi kinyume na vifungu vya Sheria hii.

(2) Katika hali yeyote ile, ikiwa kibali cha uingizaji au usafirishaji wa bidhaa kimetolewa mwanzo au kabla ya Sheria hii kuanza kufanya kazi kuhusiana na bidhaa hizo zilizoelezewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha Sheria hii, kibali kitahesabika kimetenguliwa kuanzia tarehe ya amri hiyo na Waziri atatoa kibali chengine ambacho kinakubaliana na vifungu vya amri hiyo.

(3) Ikiwa usafirishaji au uingizaji wa bidhaa au aina maalum za bidhaa zilizopigwa marufuku moja kwa moja au zilizoekewa vikwazo na amri iliyofanywa chini ya kifungu hichi, hivyo mtu yeyote ambae atasafirisha, ataingiza bidhaa au atadhamiria kusafirisha au kuingiza bidhaa ambazo zinazoenda kinyume na amri hiyo au kifungu chochote itakuwa ametenda kosa dhidi ya Sheria hii.

Utoaji wa kibali.

36.(1) Kibali kilichokuwa halali kitatolewa kwa ada ya usafirishaji au uingizaji wa bidhaa wakati na sehemu ya uingizaji au usafirishaji wa bidhaa zinazodhibitiwa na hicho kibali.

(2) Kamishna wa Forodha au mbadala wake anaweza kukataa kuruhusu usafirishaji au uingiza wa bidhaa zinazodhibitiwa zinazohusiana na kibali hicho isipokuwa kibali hicho kimetolewa pamoja na ushuru wa usafirishaji mlangoni na haitokuwa kosa kisheria kwa Kamishna au Afisa Forodha yeyote kwa sababu ya kukataa huko .

Ukatazaji wa usafirishaji wa bidhaa bila ya kibali cha Waziri.

37. Hakuna Mtu atakaengiza, kusafirisha au kusarifisha tena bidhaa kwa mfumo mwengine wowote nje ya Zanzibar bila ya kupata kibali cha Waziri.

Isipokuwa kwamba kifungu hakitatumika: kwa bidhaa zilizonunuliwa kwenye maduka ya viwanja vya ndege au katika maduka ya sehemu ya forodha na ambazo zina ushahidi wa risiti za maduka yaliyotajwa, bidhaa za nguo na bidhaa binafsi na ambazo afisa wa forodha ataridhika kuwa ni kwa matumizi binafsi.

Utaratibu wa kusafirisha bidhaa.

38. (1) Mtu yoyote ambae amekusudia kuingiza, kutoa au kutoa mzigo yoyote tena kwa mfumo mwengine nje ya Zanzibar ataomba kwa Wizara ruhusa hiyo.

(2) Baada ya maombi hayo Wizara inaweza kutoa kibali cha kuingiza, kusafirisha au kusafirisha tena kwa mfumo mwengine wa bidhaa nyengine yoyote nje ya Zanzibar.

SEHEMU YA NANE
BIDHAA ZILIZOZUILIWA NA ZILIZOPINGWA MARUFUKU

Bidhaa zilizopigwa marufuku na kuzuiliwa.

39.(1) Bidhaa zilizoanishwa kwenye jadweli ya kwanza ni bidhaa zilizopigwa marufuku pamoja na uingizwaji wake.

(2) Bidhaa zilizoanishwa kwenye jadweli ya pili ni bidhaa zilizozuiliwa na iungizwaji wake au usafirishwaji pamoja na, uhifadhi wake,

kwa mujibu wa masharti yoyote ambayo yanarekebisha uingizwaji hua nayo pia umepigwa marufuku.

(3) Bidhaa zilizoanishwa kwenye jadweli ya tatu ni bidhaa zilizozuiliwa pamoja na usafirishwaji wake nje.

(4) Waziri anaweza kuamrisha kwa kuchapishwa kwenye gazeti kwa kufanya marekebisho ya jadweli au kutangaza uingizwaji au uhusiano wa bidhaa yoyote au aina za bidhaa.

(a) zimepigwa marufuku au zimezuiliwa aidha kwa ujumla wake au kwa uhusiano wananchi yeyote maalum.

(b) zimepigwa marufuku au zimezuiliwa uhifadhi wake kutokana na masharti yoyote yanayodhibiti uingizwaji wake au kwa uhusiano wa nchi yeyote maalum.

(5) Katika utumiaji wa uwezo wake chini ya kifungu hichi, Waziri atafuata sheria ya jumuiya ya Africa Mashariki ya Uongozi wa Forodha ya toleo jipya na Sheria yoyote ya Jumuiya yenye uhusiano nayo.

Bidhaa zilizopigwa marufuku na kuzuiliwa kusafirishwa.

40.(1) Bidhaa zilizoanishwa kwenye jadweli ya tatu ni bidhaa zilizopigwa marufuku pamoja na usafirishwaji wake.

(2) Bidhaa zilizoanishwa kwenye jadweli ya nne ni bidhaa zilizozuiliwa na usafirishwaji wake, pamoja na uhifadhi wake kutokana na masharti yoyote yanayodhibiti usafirishwaji pia nao umezuiliwa.

(3) Waziri anaweza, kwa kuagiza ndani ya Gazeti, kurekebisha jadweli kwa lengo la kuweka wazi usafirishaji wa bidhaa zozote au bidhaa za aina yoyote.

(a) hairuhusiwi aidha kiujumla au kwa kuhusiana na nchi maalum;

(b) hairuhusiwi kuhifadhi kutoka na masharti yoyote yanayodhibiti usafirishaji wake aidha kwa ujumla au kwa uhusiano na nchi maalum.

Uingizaji wa mizigo kwa usafirishaji.

41.(1) Hifadhi yoyote itakayotolewa na Sheria za Forodha mizigo yote itakayopakiwa kwa kusafirishwa kwa ndege yoyote au chombo cha majini utaingizwa na mmiliki wa mzigo kwa mfumo utakaoelezwa.

(2) Endapo mmiliki atapeleka waraka wa kuingiza bidhaa chini ya kifungu hichi, atawasilisha kwa ofisi husika maelezo ya kutosha yanayoungwa mkono na ushahidi wa maandishi wa bidhaa zilizoainishwa katika nyaraka za kuingia bidhaa.

(3) Mtu yeyote atoenda kinyume na kifungu hichi, itakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia bidhaa zake zitataifishwa.

Uwezo wa ofisi wa forodha

42.(1) Ofisa wa forodha anaweza kukataa kuruhusu uingizwaji wowote uliozuiliwa au uingizwaji wa bidhaa zozote ambazo uingizwaji huo umewekewa mipaka chini ya Sheria hii mpaka ruhusa ya uingizwaji huo

itakapotolewa na yeye kuhusiana na bidhaa hizo na mpaka akaridhika kwamba uingizwaji wa bidhaa hizo hautopingana na masharti yoyote ya ruhusa hiyo.

(2) Ofisa wa Forodha anaweza kukataa kuruhusu usafirishwaji wowote wa bidhaa zilizozuiliwa au bidhaa zozote ambazo zimeekewa mipaka chini ya kifungu 45 mpaka ruhusa ya usafirishaji itakapotolewa kwake inayohusiana na bidhaa hizo na akaridhika kwamba usafirishwaji wa bidhaa hizo hautopingana na masharti yoyote ya ruhusa hiyo.

(3) Ofisa wa forodha atakataa kuruhusu uingizwaji au utoaji wa bidhaa yoyote ambayo uingizwaji au usafirishaji umepigwa marufuku kwa amri yoyote iliyofanywa na vifungu vya Sheria hii, au ikiwa chini ya vifungu hivyo uingizwaji au usafirishwaji wa bidhaa umewekewa masharti maalum, atakataa ruhusu uingizwaji au usafirishwaji wao kwa hali yoyote itakivyokuwa, mpaka atakaporidhika kwamba masharti yametekelezwa.

SEHEMU YA TISA
MAKOSA NA ADHABU

Kufanya biashara sehemu isiyoruhusiwa

43. Mtu yoyote ambae atafanya biashara au atatoa bei ya bidhaa kwa ajili ya kuuza au atatoa huduma au biashara katika sehemu ambayo.

(a) haikutosheleza mahitaji yaliyoainishwa;

(b) haikuzisambaza habari kama zinavyotakiwa na Sheria hii; au

(c) haikukusudiwa kufanywa biashara endapo mtu huyo akifanya moja kati ya mambo hayo itakuwa amefanya makosa chini ya Sheria hii na endapo akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania 300,000/= na isiyozidi 1,000,000/=

Makosa yanayohusiana na masharti ya bidhaa na huduma.

44. Mtu yoyote ambae muuzaji, mfanyabiashara au msimamizi wa biashara ambazo zinakiuka vifungu vya Sheria vinavyo husiana na asili, aina, vipimo au huduma za kuuza au utoaji wa bei kwa ajili ya kuuza tofauti na sababu na kwenye sehemu tofauti akafanya makosa chini ya Sheria hii na endapo akipatikana na hatia awajibike kulipa faini isiyopungua Shilingi za kitanzania 500,000/= na isiyozidi 1,000,000/=.

Makosa yanayohusiana na Waraka inayofuatana.

45. Mtu yoyote ambae muuzaji, mfanyabiashara au msimamizi wa biashara ambazo zinakiuka vifungu vya Sheria hii vinavyohusiana na uundaji au upatikanaji wa waraka kama atakavyotakiwa na Sheria na atakaposhindwa kutoa au kuwasilisha waraka inayofuatana kama alivyotakiwa na Sheria hii atakuwa amefanya kosa na endapo akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini ya Shilingi za kitanzania 200,000 na isiyozidi 500,000.

Kutokuwa na kibali au usafirishaji wa bidhaa.

46. Mtu yoyote ambae anaenda kinyume na masharti yoyote yanayohusiana na usafirishaji au uingizaji wa bidhaa zinazosimamiwa na ruhusa yoyote itakuwa amefanya kosa na endapo akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua 1,000,000 na isiyozidi 5,000,000 Tsh.

Kutoa taarifa za uongo

47. Mtu yoyote ambae kwa lengo la kupata ruhusa yoyote chini ya Sheria hii.

(a) akatoa tamko au maelezo ambayo ya uongo katika hali yoyote maalumu; au

(b) kutoa waraka ambao.

(i) vifaa/nyenzo yoyote maalum ya uongo.

(ii) haujawasilishwa na mtu ambae amepaswa hasa kuwasilisha au

(iii) ushabadilishwa kwa njia yoyote ile.

Bila kuathiri aina yoyote ile ya adhabu ambayo itakayotolewa na Sheria nyengine yoyote, isipokuwa imethibitisha kwamba amechukuwa hatua zote muafaka kuhakikisha kwamba tamko au maelezo yaliyotolewa au yaliyokuwemo kwenye waraka wowote uliyotolewa na yeye kuwa ni wakweli au na akaridhika kuwa waraka aliyoutoa ni waraka halisi. Atakuwa kutokuwa amefanya makosa na endapo akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua Tanzania shilingi 500,000 na isiyozidi shilingi 1,000,000.

Ni marufuku kumpa mtu mwengine kibali.

48. Mtu yeyote aliyepewa kibali cha kuingiza au kusafirisha bidhaa au kutoa huduma hatoruhusiwa kumpa mtu mwengine kibali hicho, isipokuwa pale ambapo kuna ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi ya kumuezesha kufanya hivyo, mtu yeyote ambae ataenda kinyume na kifungu hichi atakuwa ametenda kosa na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Tanzania Shilingi 500,000 na isiyo zidi 1,000,000.

Uingizaji, utoaji/ usafirishaji wa namna nyengine wa bidhaa zilizopigwa marufuku

49. Mtu yoyote aliyekusudia kuingiza, kusafirisha au kuzisafirisha tena kwa namna nyengine yoyote ya bidhaa zozote zilipigwa marufuku na Sheria hii itakuwa amefanya makosa na endapo akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi 500,000 au kifungo kisichozidi mwaka mmoja.

Adhabu

50. (1) Mtu yoyote ambae atafanya kosa lolote chini ya Sheria hii au Kanuni zilizofungwa chini ya Sheria hii ambayo adhabu zake hazijaonyeshwa / kuelezwa atakuwa ni mkosa na akipatikana na hatia atatozwa faini Tanzania isiyopungus Shilingi 100,000 na isiyozidi 300,000 au kifungu kisichopungua mwaka mmoja.

(2) Endapo mtu ameadhibiwa kwa kosa lolote dhidi ya Sheria hii, itakuwa halali kwa mahakama ambayo imemtia hatiani mtu huyo kuzitaifisha bidhaa zinazohusiana na adhabu hiyo.

Adhabu za papo hapo.

51.(1) Endapo Mkurugenzi anazo sababu za kuamini kwamba mtu yoyote ametenda au anatenda kosa ambalo Sheria imelionesha kuwa ni kosa, Mkurugenzi anaweza kumpa taarifa ya maandishi yenye kuonesha kwamba anatiwa hatiani kwa kosa lake hilo kwa kulipa faini kwa adhabu ya papo

hapo na mtu huyo hatokuwa tena mwenye hatia kwa kosa hilo ikiwa adhabu ya papo hapo imetekelezwa kwa mujibu wa kifungu hichi cha Sheria hii kabla ya kumalizika kwa siku 14 baada siku iliyotolewa taarifa (notisi) hiyo au kabla ya siku ambayo shauri halijaanzwa kusikilizwa Mahakamani kwa tukio lililotokezea.

Isipokuwa mtu huyo aliyedhibitiwa chini ya kifungu hichi sio Mzanzibari au sio mkaazi wa Zanzibar, adhabu ya papo hapo itatakiwa ilipwe mara tu baada ya tukio.

(2) Endapo mtu amepewa taarifa (notisi) chini ya kifungu hiki kuhusiana na kosa, mashtaka hayatochukuliwa dhidi ya mtu huyo kwa kosa hilo mpaka na baada ya kumalizika siku kumi na nne tokea tarehe ya taarifa (notisi) hiyo.

(3) malipo ya adhabu ya papo kwa hapo chini ya kifungu hichi yatafanywa na Mkurugenzi au mtu yoyote atakae chaguliwa na Waziri kwa agizo lililochapishwa kwenye Gazeti na malipo yatakayolipwa kwa njia hiyo yatachukuliwa kama ni faini iliyotolewa na kosa hilo.

(4) taarifa chini kijifungu hichi cha kifungu hichi zitaainishwa makosa yanayodaiwa na kutoa maelezo ya msingi dhidi ya makosa hayo na pia itaeleza muda ambao matukio hayo hayatochukuliwa kuwa ni makosa kiwango cha adhabu ya papo hapo, na kuwaainisha maofisa ambao adhabu ya papo hapo wanaoweza kulipwa.

Makosa yanayofanywa na makampuni, mashirika nk.

52. Endapo makosa yamefanyika na makampuni au mashirika au jumuiya kila Mkurugenzi, Maofisa husika wa Kampuni hiyo, kila mbia, maofisa wa mashirika na mtu yoyote anaehusiana na uongozi wa jumuiya hizo kila mmoja atashitakiwa na kuadhibiwa kwa kosa kwa mfumo huo huo kana kwamba yeye ndie aliyetenda kosa hilo, isipokuwa kufanya au kuacha kufanya inajumuisha makosa yaliyotokezea bila kujua, ridhaa au kula njama.

Rufaa

53. (1) Mtu yoyote asiyeridhika na hukumu iliyotolewa na Sheria hii anaweza kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Kila rufaa itatakiwa iwe kwa maandishi na iwasilishwe kwa wakati kama ilivyoelezwa na kanuni.

(3) Maamuzi ya Waziri katika hali yoyote ile yataathiriwa na ukataji wa rufaa juu ya maamuzi hayo.

(4) Mtu ambae hakuridhika na maamuzi ya Waziri anaeweza kukata rufaa yake kwenye Mahakama kuu, na maamuzi ya Mahakama kuu yatakuwa ya mwisho.

Uwezo wa kutunga kanuni.

54.(1) Waziri anaweza kutunga kanuni.

(a) kuhusiana na utoaji wa ruhusa kuhusiana na uingizwaji na usafirishwaji wa bidhaa zilizoainishwa kwenye notisi / taarifa, pamoja na masharti ya uombaji wa vibali hivyo;

(b) kuhusiana na urekebishaji na udhibiti wa uigizwaji na usafirishwaji wa mizigo;

(c) kuhusiana na urekebishaji wa ufanyaji wa biashara yoyote, ikiwa kwa jumla au reja reja;

(d) kuhusiana utowaji wa bidhaa au aina yoyote ya bidhaa kwa ufanisi na kwa uadilifu;

(e) kuhusiana na utaratibu, ulinganishaji na usimamiaji wa masoko ya biashara pamoja na maonyesho ya biashara;

(f) kuhusiana uelezaji wa fomu zinazotumika na Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

55.(1) Sheria zifuatazo zinafutwa.

(a) sheria ya biashara Zanzibar Nam. 4 ya 1989;

(b) sheria ya kuzuia Magendo Nam. 5 ya 1986;

(c) kanuni za Sheria za biashara ya mwaka 1980.

(2) Bila kuathiri Sheria zilizofutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha Sheria hii Kanuni zote na chochote kilichofanywa chini ya Sheria zilizofutwa kabla ya Sheria hii kuanza kutumika zitachukuliwa kuwa kama zimefanywa na Sheria hii mpaka Sheria ndogo ndogo zitakapofutwa na kuweka nyengine badala yake.

MADHUMUNI NA SABABU

Mswada huu lengo lake kuu kukuza biashara Zanzibar kwa kuweka mfumo wa kisasa wa biashara utakaoweza kukizi mahitaji muhimu yatakayoweza kukuza kipato kwa Serikali lakini pia kuleta mafanikio kwa wafanya biashara.

Shughuli za biashara ndio uti wa mgongo wa uchumi na maisha ya watu wa Zanzibar. Kwa karne nyingi biashara imeshamiri Zanzibar na imekuwa ikiongozwa na Sheria na Kanuni mbali mbali. Sheria hizo zimekuwa zikiongoza zaidi leseni, ruhusa za kufanya biashara na mapato.

Kwa muda wote huo hapakuwa na Sheria mahsusi ya kuongoza mambo kadhaa ambayo ni muhimu katika ufanyaji wa biashara. Miongoni mwa mambo hayo ni:

(a) uingizaji bidhaa;

(b) udhibiti wa bidhaa;

(c) kukataza baadhi ya biashara au bidhaa kuingizwa;

(d) utaratibu wa kufanya biashara na mengineyo.

Sheria Biashara Namb. 4 ya 1989 inaonekana wazi kuwa ina mapungufu mengi yenye msingi kisheria, hivyo mswaada huu umekuja kwa wakati muafaka ili kuja kuondosha mapungufu hayo pamoja na kuboresha shughuli za kibiashara Zanzibar.

Mswaada huu umegawika sehemu tisa :

Sehemu ya kwanza: inahusiana na jina fupi na kuanza kutumika, eneo la matumizi na ufafanuzi.

Sehemu ya pili: inahusioana na kuanzishwa kwa idara yenye majukumu ya biashara na uteuzi wa Mkurugenzi na kazi za idara.

Sehemu ya tatu: inahusiana na kuanzishwa kwa baraza, muundo wa baraza, kazi za baraza, mkutano wa baraza, fedha za baraza na taarifa ya mwaka.

Sehemu ya nne: inahusiana na mamlaka ya usimamizi, uwezo wa wasimamizi na amri kutoka kwa wasimamizi.

Sehemu ya tano: inahusiana na usajili wa biashara, utoaji wa leseni za biashara, mipaka ya mamlaka ya leseni ya biashara, ombi la usajili wa biashara na kazi za mamlaka ya utoaji wa leseni.

Sehemu sita: inahusiana na uuzaji wa bidhaa, wajibu wa mfanya biashara, wajibu wasimamizi wa biashara, wajibu wa muuzaji, mambo ya kuzingatia katika uuzaji wa bidhaa na utoaji huduma, kufanya biashara za mtaani, ufanyaji bishara sokoni, kufanya biashara kwenye sehemu za wazi, mambo ya kuzingatia katika utoaji wa vibali na upunguzaji wa bei wa bidhaa.

Sehemu ya saba: inahusiana na bidhaa zenye kudhibitiwa, ombi la kupewa kibali cha uingizaji au usafirishaji wa bidhaa, utoaji wa kibali, utoaji wa kibali cha uingizaji na usafirishaji wa bidhaa au huduma nyengine yeyote, utenguaji wa kibali, uwezo wa waziri kupiga marufuku au kuweka mipaka ya uingizaji au usafirishaji wa bidhaa, utoaji wa kibali, ukatazaji wa usafirishaji wa bidhaa bila ya kibali cha waziri na utaratibu wa kusafirsha bidhaa.

Sehemu ya nane: inahusiana na bidhaa zilizopigwa marufuku na kuzuiliwa, bidhaa zilizopigwa marufuku na kuzuilliwa kusafirishwa, uingizaji wa mizigo kwa usafirishaji na uwezo wa ofisa wa forodha.

Sehemu ya tisa: inahusiana na kufanya biashara sehemu isiyoruhusiwa, makosa yanohusiana na masharti na bidhaa na huduma, makosa yanayohusiana na waraka inayofuatana kutokuwa na kibali kwa uingizaji au usafirishaji wa bidhaa, ni marufuku kumpa mtu mwengine kibali, kutoa taarifa za uongo, uingizaji, usafirishaji au usafirishaji wa namna nyengine wa bidhaa zilizopigwa maarufuku, adhabu za papo hapo, makosa yanayofanywa na makapuni , mashirika nk., rufaa, uwezo wa kutunga kanuni

na kufuta na kubakiza Sheria ya biashara Zanzibar Namb 4 ya 1989 na Sheria ya kuzuia magendo Namb. 5 ya 1986 na kanuni ya Sheria ya biashara ya 1980.

JADWELI LA KWANZA

(Chini ya Kifungu cha 39(1))

BIDHAA ZILIZOPIGWA MARUFUKU

1. Bidhaa zote zinazoingizwa ambazo zimepigwa marufuku chini ya Sheria yote inayofanyakazi Zanzibar kwa wakati huu.

2. Pesa Bandia, Peasa Haramu, aina zote za pesa ambazo zilizoanzishwa kwa viwango maalum.

3. Bidhaa za aina ya ngono katika mfumo wote wa mawasiliano kukashifu, zilizochapishwa, kutiwa rangi, mabuku ya ngono, kadi za ngono na mambo mengine yoyote ya udhalilishaji.

4. Vibiriti vinavyotengenezwa kwa white *"phosphorous"*.

5. Aina ya vinywaji vyenye kumiminika ambayo imejumuisha mafuta au bidhaa za kikemikali ambazo zinaathari kwa afya ya mwanadamu, ikijumuisha "thijone", "star arise", "benzoic aldehyde", "salicyclic esters", "hyssop and absinthe". Isipokuwa kwamba hakuna kitu katika sehemu hii itatumika "Anise and Anisette" vinywaji ambavyo vimejumuisha sio zaidi ya 0.1% ya mafuta ya "Anise and distillates from either pimpinella anisum or the star arise allicium verum".

6. Madawa ya kulevya chini ya usimamizi wa kimataifa.

7. Uchafu na mabaki yake ambayo yapo chini ya mikataba ya kimataifa.

8. Sabuni za aina zote bidhaa za mapambo ambazo zina "mercury".

9. Maringi yanotumika kwa vyombo vya biashara na gari zamizigo na gari za abiria.

10. Bidhaa za kilimo na kemikali za viwandani:

    (a) kemikali za kilimo;

        (i) 2.4 - T;

        (ii) Aldrin;

        (iii) Caplafol;

(iv) Chlordirneform 1 Chlorobenxilate 1 DDT

(v) Dieldrin;

(a) - Dibroacethanel (EDB)

(vi) Flouroacelamide;

(vii) Hexachlorocylohexane (HCH);

(viii) Hiplanchlor;

(ix) Hoscachlorobenzene;

(x) Lindone;

(xi) Mercury compounds;

(xii) Monocrolophs (certain formulations);

(xiii) Methamidophos;

(xiv) Phospharrmion;

(xv) Methyl - parathion;

(xvi) Parathion.

(b) Kemikali za Viwandani:

(i) Crocidolite;

(ii) Polychlorominatel biphenyls (PBB);

(iii) Polyuchlorinated Biphenyls (PCB);

(iv) Polychlororinated Terphyenyls (PCT);

(v) Tris (2.3 dibromopropyl) phosphate;

(vi) Methylbromide (to be phased out in accordance with the Montreal Protocol by 2007).

11. Bidhaa za bandia za aina yoyote zilizofanyiwa marekebisho na L.N. EAC/13/2008 tarehe 30/6/2008.

JADWELI LA PILI
(Limetengenezwa chini ya kifungu 39(2))

BIDHAA ZILIZOPIGWA MARUFUKU

1. Bidhaa zote ambazo uingizwaji wake ambao unaongozwa na Sheria hii au Sheria nyengine yeyote inayofanya kazi ndani ya Nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

2. Huduma za mashine za kiposta isipokuwa kwa masharti ya kibali cha maandishi kilichotolewa na mamlaka yenye uwezo ya Nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

3. Vitu vyenye mazingira kusababisha mauwaji au kukamata wanyama ya aina yeyote na isipokuwa kwa masharti ya kibali cha maandishi kilichotolewa na Nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

4. Bidhaa zenye thamani ya chuma au mawe.

5. Silaha na mirupuko iliyoainishwa katika sura ya 93 ya forodha.

6. Mabaki na mifupa kwa tindi kali.

7. Mfupa mengine na pembe na bidhaa nyengine zinazotokana na hizo.

8. Tembo, pembe zilizotaarishwa lakini hazijawekwa katika maumbile.

9. Vifaru, meno yailizotarishwa lakini hazijawekwa katika maumbile.

10. Kiboko, Pembe, zilizotaarishwa lakini hazijawekwa katika maumbile.

11. Au pembe nyengine zilizotengenezwa.

12. Unga wa pembe na mabaki.

13. Magamba ya Kobe, na mabaki ya nyangumi.

14. Matumbawe na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

15. Sponji la asili la Wanyama.

16. Vitu vya mafuta yaliyotumika na nyukilia.

17. Pembe zilizotumika.

18. Mifupa, magamba ya Kobe, matumbawe na mabaki mengine ya Wanyama.

19. Ozone Depelting Substances under the Montreal Protocol (1987) and the Vienna Convention (1985).

20. Genetically modified products.

21. Aina asilia za Samaki na mayai.

22. Aina zilizopo hatarini kupotea duniani.

23. Biashara ya maringi yalokwisha tumika.

24. Madawa yote yaliyokatazwa chini ya udhibiti wa kima Taifa.

25. Mambo yanayohusiana na kihistoria.

26. Bidhaa zilizoanishwa katika sura ya 36 ya sheria inayohusiana na forodha ya Jumuiyaya Afrika Mashariki.

27. Sehemu za silaha na miripuko pamoja na vyuma.

28. Vyombo vya kivita vinavyoongozwa na 8710 na mambo yanayohusiana na ushuru wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

29. Darubini na mambo mengine yanayosaidia kuona ambazo ni muafaka kwa matumizi ya kijeshi kama yalivyoanishwa katika sura ya 90 ya Sheria inayohusiana mambo ya foroza ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

30. Mishare na mambo mengine yanayohusiana na hayo kama yalivyoanishwa chini ya sura ya 95 ya Sheria inayohusiana na forodha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

31. Vipande vilivyookotwa vya silaha na miripuko vinavyoongozwa na No 9705 au 9706 ya Sheria inayohusiana na forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

ZANZIBAR
8 Julai, 2013

(NASSOR AHMED MAZRUI)
Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzbar